

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA KUPATA MAONI YA WADAU KUHUSU MABADILIKO YA KANUNI
YA KUPANGA NA KUKOKOTOA BEI YA BIDHAA ZA MAFUTA ILI KUONGEZA
KANUNI YA KUKOKOTOA BEI YA GESI YA KUPIKIA**

Kwakuwa biashara ya gesi ya kupikia ilikuwa haijakua sana ikiwa ni pamoja na matumizi kidogo na kutokuwepo kwa miundombinu (ya kuhifadhia) inayotosheleza, EWURA ilifanya udhibiti wa kiufundi katika gesi ya kupikia. Hivyo basi, Kampuni za Gasi ya Kupikia (LMCs) zilikuwa zinapanga bei ya gesi ya kupikia kulingana na soko lao ili kuziwezesha kujitangaza na kuongeza masoko pamoja na kujenga miundombinu ya kuhifadhia na usambazaji wa gesi ya kupikia.

Ikumbukwe kuwa mwaka 2013 na 2016, EWURA ilifanya taftishi ili kurekebisha kanuni kwa kuongeza kanuni ya kukokotoa bei ya gesi ya kupikia. Wakati wa taftishi ilifahamika kuwa miundombinu ilikuwa haitoshelezi, matumizi ya gesi yalikuwa chini na pia kulikuwa hakuna viwango vinavyojulikana vya gesi ya kupikia pamoja na miundombinu.

Pamoja na hayo, kumekuwepo na malalamiko kuwa bei ya gesi ya kupikia ipo juu na hivyo inatakiwa kudhibitiwa na EWURA. Ifahamike kuwa EWURA imeendelea kufatilia bei ya gesi kila wakati na ilipobidi iliweza kuingilia upangaji bei ili bei iwe halisia.

Kutokana na hayo, EWURA inapendekeza mabadiliko katika Kanuni za Kupanga Bei za Mafuta ili kuanza kupanga na bei za gesi ya kupikia (LPG).

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA Na. 414, EWURA inaanziha mchakato wa kupata maoni ya wadau kuhusiana na pendekezo la kanuni mpya ya kukokotoa bei za bidhaa za mafuta itakayojumuisha gesi ya kupikia Katika mchakato huo, EWURA itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Kampuni za Kuuza Gesi ya Kupikia (LMCs); Wasambazaji na Wauzaji rejareja wa gesi ya kupikia, Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) pamoja na wananchi wote kwa ujumla.

Mkutano wa Taftishi wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau utafanyika tarehe **13 Septemba 2018** katika Ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki kuanzia **saa tatu na nusu (3.30) asubuhi**. Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kumwandikia Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonyeshwa hapo juu kabla ya **14 Septemba 2018** au kupitia barua pepe info@ewura.go.tz. Wadau watakaopenda kupewa muda wa kuwasilisha maoni yao katika mkutano wa wadau wanatakiwa kuonyesha nia yao kwa kuiandikia EWURA ifikapo tarehe **10 Septemba 2018**.

Mamlaka imeandaa Muhtasari wa Majadiliano kuhusiana na mada hii. Nakala za Muhtasari huu zinapatika katika Ofisi za Mamlaka Makao Makuu na katika Ofisi za Kanda wakati wa muda wa kazi kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni. Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa wa kutoa maoni yao ili kufanikisha zoezi hili. Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kumwandikia Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo juu.

Limetolewa na

Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji